# DARUBINI

## Uwezeshaji wa Wanawake katika Sekta ya Uziduaji Tanzania.



©HakiRasilimali

Toleo la 4
Aprili 2024

Imedhaminiwa na: Belgium partner in development

Imechapishwa na:
HakiRasilimali, International Peace Information Services (IPIS),
Business Human Rights Tanzania (BHRT) & Avocats Sans Frontières (ASF)

## Utangulizi

Sekta ya uziduaji Tanzania, hujumuisha sekta ya madini, mafuta na gesi, ambayo hutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi. Shughuli za uziduaji sio tu huongeza mapato ya nchi lakini pia huathiri ustawi wa watu. Hata hivyo bado kuna changamoto kubwa kuhusu usawa wa mgawanyo wa faida zinazo tokana na sekta kwenda kwa makundi yote ya jamii, hususani wanawake. Katika sekta ya madini wanawake kwa kiasi kikubwa huangukia katika makundi yafuatayo: wale wanaomiliki mashimo na leseni za uchimbaji madini, watoa huduma, waongezaji thamani, na wachenjuaji; wale walioajiriwa katika majukumu yenye uhitaji wa ujuzi na hata yasiyo na uhitaji wa ujuzi; na wale wanaoishi katika maeneo ya uchimbaji wa madini, wanaoathirika na shughuli za uchimbaji madini.

Licha ya juhudi za kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake katika nyanja mbalimbali za jamii, bado kuna ufinyu katika ushiriki na uwakilishi wa wanawake katika sekta ya uziduaji (UN Women, 2016) Ajira katika sekta ya uziduaji nchini Tanzania imetawaliwa kwa wingi na wanaume, huku tofauti kubwa ya kijinsia ikionekana kukaribia 80% (TEITI, 2021)

Wanawake wanakabiliwa na changamoto kubwa zinazozuia ushiriki wao kikamilifu na wenye manufaa. Wanakumbana na hali ya kutengwa na kukutana na vizuizi haswa vya kimifumo vinavyotokana na mambo ya kisheria, kitamaduni, kijamii na kiuchumi. Vikwazo hivi vinawaweka wanawake kwenye ukingo wa michakato ya kufanya maamuzi, na huzuia upatikanaji wa fursa za maendeleo ndani ya sekta ya uziduaji (HakiRasilimali, 2024)


Kulingana na mifumo iliyopo haswa mifumo ya kisheria na kisera, ripoti hii inatoa mwanga juu ya changamoto zinazowakabili wanawake nchini na umuhimu wa kukuza sekta ya uziduaji inayozingatia jinsia.

## Ushiriki wa Wanawake katika Sekta ya Uziduaji

Benki ya Dunia imetoa ripoti mwaka 2023 kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na imetoa picha ya kuogopesha kuhusu lengo namba tano (SDG 5): "Kufikia Usawa wa kijinsia na Kuwawezesha Wanawake na Wasichana Wote". Ripoti imeonesha kwamba dunia iko mbali sana katika kufikia usawa wa kijinsia ifikapo 2030, na kwa kasi hii itachukua miaka 300 kukomesha ndoa za utotoni, miaka 286 kuziba mianya ya ulinzi wa kisheria na sheria za kibaguzi, na miaka 140 kupata uwakilishi sawa katika uongozi na kazi UN, 2023)

Ripoti ya mwaka 2023 ya Tanzania Extractive Industries Transparency Initiatives (TEITI) haijazingatia sana masuala ya jinsia lakini inabainisha kuwa ushiriki wa wanawake katika suala la ajira zinazotolewa na makampuni ya uziduaji ni chini ya 10% (TEITI, 2021) Kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), sekta ya madini na uchimbaji mawe ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa gesi asilia ilitoa mchango mkubwa wa ajira katika mwaka wa fedha 2020/21, ajira za moja kwa moja zilikua ni 218,353, wanaume 176,815 na wanawake 41,538 (20%)(TEITI, 2023). Ingawa vipimo katika ripoti zote mbili ni tofauti, bado kuna tofauti kubwa ya kijinsia.

Hili linadhihirika wazi wakati wa kukagua nguvu kazi ya kampuni tano bora za uchimbaji madini nchini Tanzania, ambazo ni Geita Gold Mine, Bulyanhulu, North Mara, na Shanta Gold Mining (tazama Mchoro 1)[3].




Ushiriki wa wanawake bado unaendelea kuwa changamoto kutokana na kuwepo kwa vikwazo vya kimuundo na kiutamaduni. Pengo hili la kijinsia hutoa taswira ambayo ni zaidi ya uwakilishi wa idadi kwamaana hugusa hadi nafasi ya kufanya maamuzi ndani ya makampuni haya na kusababisha sera ambazo huweka kando uzoefu na maslahi ya wanawake katika miradi ya uziduaji (Oxfam, 2016). Mwenendo huu unadhihirika katika sekta ya madini nchini Tanzania. Ripoti ya TEITI inaonyesha tofauti kubwa ya ajira katika idadi ya wanaume na wanawake katika makampuni ya uziduaji.

## Changamoto ya Kisera

Ripoti ya Benki ya Dunia ya 2023 inasisitiza umuhimu wa kuanzisha mifumo ya kisheria inayolinda haki za wanawake kama hatua ya msingi katika kupambana na ubaguzi dhidi yao katika sekta ya uziduaji (Wold bank, 2023)

Kutokuwepo kwa tamko mahususi la sera kuhusu ushiriki wa wanawake katika sekta ya uziduaji ndani ya (Sera ya madini ya Tanzania, 2009) kunaonyesha mapungufu mkubwa.

Kuweka kipaumbele kwa mkakati ulio wazi wa kijinsia ni muhimu ili kuwezesha na kuongoza hatua madhubuti zinazolenga kufikia usawa wa kijinsia katika sekta ya uziduaji.

Zaidi ya hayo, kuna haja ya kurejea kanuni za ushirikishwaji wa wazawa kwani kwa sasa hazina miongozo (masharti) ya ujumuishi wa kijinsia. Kwa mfano, wakati Kampuni ya Madini[1] imeteua idadi kubwa ya Watanzania katika nafasi za uongozi, uwakilishi wa wanawake katika nafasi hizo bado ni mdogo sana. Kulingana na hayo, kuna umuhimu mkubwa wa kurekebisha kanuni hizi ili kushughulikia changamoto zinazowakabili wanawake katika ajira.

Pia, katika mashirika ya serikali bado kuna nafasi kubwa ya kuboresha na kuhakikisha uwakilishi na usawa wa kijinsia, kama inavyoonyeshwa na muundo wa Tume ya Madini. Jambo la kusikitisha ni kwamba muundo wa Tume ya Madini na kamati zake chini ya Sheria ya Madini haujali jinsia.

Tume ya Madini inaundwa na Mwenyekiti, Katibu Mkuu (Hazina), Katibu Mkuu (Wizara ya Ardhi); Katibu Mkuu (Wizara ya Ulinzi); Katibu Mkuu (Wizara ya Serikali za Mitaa); Mtendaji Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Madini Tanzania; Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na watu wawili ambao wana ujuzi na uzoefu uliothibitishwa katika sekta ya madini, mmoja wao anapaswa kuwa mwanamke.

Kwa hali ilivyo, Muundo wa Tume ya Madini unahitaji uwepo wa mwanamke mmoja pekee na wajumbe wengine wanaojiunga nayo kwa nafasi zao rasmi (wengi wao wakiwa Makatibu Wakuu wa Wizara) si kwa uwakilishi wa jinsia (HakiRasilimali 2021)

"Tunahitaji juhudi za makusudi zenye ufanisi (zilizowekwa katika maandiko na mfumo) ambazo zinaonyesha utashi wa kisiasa, na mfumo wa kisheria wa kuwawezesha wanawake".

Bw. Stephen Aloys - GEPC

## Mapendekezo katika Kushughulikia Changamoto za kijinsia katika Sekta ya Uziduaji

- Kurekebisha Sheria ya Madini ili kurekebisha muundo wa Tume ya Madini, na kusisitiza usawa wa kijinsia. Hii inajumuisha marekebisho ya vigezo vya kuwepo katika tume ili kuleta uwakilishi mzuri wa kijinsia, na hivyo kuhakikisha wanawake wanachukua sehemu kubwa ya nyadhifa ndani ya Tume.
- Kuna haja ya kupitia upya Sera ya Madini ya 2009 na kuleta mitazamo ya kijinsia katika mahitaji ya ushirikishwaji wazawa na viwango vya ajira ndani ya makampuni ya uchimbaji madini. Hii itasaidia katika kupunguza tofauti za kijinsia katika sekta.
- Kuhimiza Makampuni na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendeleza mipango ya kuwawezesha wanawake kama sehemu ya programu za Majukumu ya Kijamii. Kuna hitaji maalumu la mipango inayolenga moja kwa moja au kuhusisha sekta ya Uchimbaji Mdogo.



Utafiti wa hivi karibuni uliofanywa na (HakiRasilimali) kwa lengo la kuelewa hali ya ushiriki wa wanawake na namna wanavyo nufaika na usimamizi wa mapato ya madini. Ripoti hio iliangazia vikwazo vya kimifumo vinavyowaweka wanawake kando ya mnyororo mzima wa thamani ya mapato ya madini. Miongoni mwa vikwazo vilivyobainishwa na utafiti huo ni mfumo wa kisheria ambao hauzingatii jinsia, upungufu wa upatikanaji wa fedha, kanuni endelevu za kijamii na kitamaduni, na fursa chache za elimu na ukuzaji ujuzi. Mwanasheria aliyehusika katika utafiti huo alisema kuwa "Ni nadra sana kukuta mwanamke akimiliki shimo la uchimbaji madini (kitalu) isipokuwa alilipata kwa njia ya urithi kutoka kwa marehemu baba au mume wake. Wale wanaoshiriki katika uchimbaji madini wanajishughulisha tu na shughuli nyingine kama vile kuchuma mabaki ya dhahabu na kuchenjua."

Upatikanaji wa mtaji ni kikwazo kikubwa kwa wanawake wanaotaka kujihusisha na kushiriki katika shughuli za uchimbaji madini. Kama ilivyothibitishwa na mmoja wa wanawake waliohojiwa katika utafiti huo ***"Changamoto yetu kuu ni mtaji. Hatuna sifa za kupata mikopo inayotolewa na mamlaka za serikali za mitaa kwa sababu mara tu unapohusika katika uchimbaji madini, unachukuliwa kuwa mwanamke mwenye uwezo wa kifedha. Taasisi za kifedha kama benki hazituamini maana uchimbaji madini ni kama kamari, hakuna uhakika kwamba mtu atapata madini hayo na kuweza kulipa mkopo huo. Kwa hiyo tumeamua kujipanga kwa kuanzisha vyama vya ushirika vya kuweka na kukopa (SACCOS). Bado haijafanya kazi, lakini tunatumai itakapoanza kufanya kazi, itatusaidia sana. Kila mwanachama atachangia kiasi cha fedha kilichokubaliwa na kuweza kukopa kwa riba nafuu".***

> "Kwa nini hakuna kipaumbele katika kauli za kisera kwa wanawake? Wanawake wametajwa tu kama suala mtambuka katika sera ya madini ya mwaka 2009"
>
> Bw. Erick Luwongo kutoka HakiMadini, alihoji kukosekana kwa msisitizo wa kisera wa uwezeshaji wa wanawake katika sekta ya madini

Ukandamizaji wa wanawake katika sekta ya uchimbaji unaendea zaidi ya changamoto za kiuchumi. Ripoti ya Benki ya Dunia imeonyesha kuenea kwa unyonyaji na unyanyasaji unaowakabili wachimbaji migodi wanawake. Changamoto ya upatikanaji wa mitaji mara nyingi huwasukuma wanawake katika majukumu ya kazi yenye malipo ya chini, wakati dhana potofu zilizoenea kuhusu nguvu, utimamu na uimara wa kimwili zinazuia zaidi fursa zao za kazi zinazolipa vizuri zaidi.

Ripoti za unyonyaji wa kijinsia na kutotendewa sawa katika suala la heshima na mishahara zimeongeza viwango vya unyanyasaji katika sekta ya madini ikilinganishwa na sekta zingine. (World bank, 2023).

Katika kukabiliana na changamoto hizo, HakiRasilimali iliendesha Kongamano la Wanawake kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani 2024, likilenga kuangazia hali ya mienendo ya kijinsia ndani ya sekta ya uziduaji. Washiriki kutoka sehemu mbalimbali walishiriki kwa kutoa uzoefu na changamoto zilizopo, washiriki waliangazia vikwazo vinavyoendelea kama vile vikwazo vya urasimu katika kupata leseni na ukosefu wa kipaumbele kwa wanawake katika mifumo ya sera.

Mshiriki kutoka Kahama, muwakilishi kutoka "Kikundi Cha Wavuja Jasho "alieleza kuwa ***"Wanawake wanakabiliwa na changamoto kadhaa hasa wale ambao wanashiriki moja kwa moja katika shughuli za uchimbaji, na kwa upande wetu, tumekuwa tukihangaika kupata leseni ya eneo ambalo tunafanya kazi, na ni muda mrefu sana mpaka sasa, na tulipouliza manispaa walijibu swala hili lipo chini ya Kamishna, tafadhali Mhe. Kamishna Msaidizi tusaidie kupata Leseni".***

Kama inavyoonyeshwa katika tafiti mbalimbali na vikao vinavyo husisha wadau wa sekta, kuna mazungumzo yanayo endelea kuhusu uharaka wa kutekeleza mikakati ya kina ili kukuza usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake ndani ya sekta ya madini.



1.Jinsi ya kuziba mianya ya kijinsia katika uchimbaji madini (Mwananchi)

2.Huduma ya afya ya uzazi ni muhimu katika uchimbaji madini, kuhamasisha ushiriki wa wanawake (Habari za kila siku)

3.Wanawake wajitosa katika sekta ya madini licha ya changamoto wanazopitia (Chanzo)

4.Sekta sita bado zina uwakilishi mdogo wa wanawake (Mwananchi)

5.Wanawake wapewa changamoto kuchangamkia fursa za sekta ya madini (Habari za kila siku)

6.Wanawake wachimbaji madini, waitishe maeneo yao ya uchimbaji (IPP Media)

7. Serikali ya Tanzania inazitaka kampuni za madini kuzingatia wanawake zaidi katika sekta ya madini (Mwananchi)




HakiRasilimali Enhancing Transparency & Accountability of the Extractive Industry in Tanzania

IPIS

BHRT BUSINESS AND HUMAN RIGHTS TANZANIA

ASF Avocats Sans Frontières